# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## Jukwaa la Watumiaji Tanzania

**Tanzania Consumer Forum (TCF)**

**TAARIFA FUPI JUU YA JUKWAA LA WATUMIAJI TANZANIA (TANZANIA CONSUMERS FORUM –TCF) TAREHE 15 MACHI 2024**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam**, Mhe. Albert J. Chalamila,**

Waheshimiwa Makatibu Wakuu wote mliopo hapa,

Waheshimiwa Wakurugenzi Wakuu, Mamlaka za Udhibiti (LATRA, EWURA, TCRA na TCAA),

Waheshimiwa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ushauri wa Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa (LATRA CCC, EWURA CCC, TCRA CCC na TCAA CCC),

Waheshimiwa Makatibu Watendaji wa Mabaraza ya Ushauri wa Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa (LATRA CCC, EWURA CCC, TCRA CCC na TCAA CCC),

Waheshimiwa Wasajili Mabaraza ya Ushindani, FCT na ZFCT,

Mheshimiwa Mkurugenzi Mkuu, ZFCC,

Waheshimiwa Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Serikali na Binafsi,

Wageni waalikwa, Wanahabari Mabibi na Mabwana,

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Awali ya yote tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai , afya na pia kwa kutujalia neema ya kukutana hapa Dar es Salaam, katika Ukumbi huu wa Karimjee kwa ajili ya maadhimisho ya kilele cha siku ya mtumiaji Duniani kwa mwaka huu, 2024.

**HISTORIA FUPI YA JUKWAA LA MTUMIAJI TANZANIA.**

**Ndg. Mgeni rasmi,**

Tunaomba kueleza kwa ufupi historia ya Jukwaa la mtumiaji Tanzania (TCF).

Kwa kutambua;

- Changamoto mbalimbali zinazowakabili watumiaji wa bidhaa na Huduma mbalimbali Nchini (Tanzania Bara na Visiwani);
- Uwepo wa Mabaraza yaliyopo kisheria na uwezo wa kutekeleza majukumu yao ya kulinda maslahi ya watumiaaji wa Huduma zinazodhibitiwa na zisizodhibitiwa;
- Jukumu la pamoja la kuhakikisha maslahi ya watumiaji yanawasilishwa kimkakati na kikamilifu katika utengenezaji wa Sera, Sheria na Kanuni zinazohusu Sekta mbalimbali Nchini;
- Mwaka 2019, viongozi wa LATRA CCC, EWURA CCC, TCRA CCC, na TCAA CCC, FCT kwa upande wa Tanzania bara na ZFCT na ZFCC kwa upande wa Zanzibar waliamua kukaa kwa pamoja na kujadili juu ya utekelezaji wa majukumu yao, na hatimaye kuona umuhimu wa kuwa na Jukwaa Moja la kuunganisha *nguvu ya kujadili na kuweka mikakati ya kutatua* changamoto mtambuka, zinazowakabili watumiaji wa Bidhaa, na Huduma mbalimbali Nchini.

**Ndg. Mgeni rasmi,**

Tangu kuanza kwa Jukwaa hili la TCF, tumekuwa na mafanikio mengi ya pamoja, ikiwa ni pamoja na:

(a) Kuwa na MoU ya majaribio ambayo kwa sasa iko katika hatua za mwisho ili iweze kusaininwa na viongozi Wakuu wa taasisi zote zinazoshirikiana katika umoja huu;

(b) Kushirikiana katika kuandaa na kuadhimisha, kilele cha siku ya mtumiaji duniani, inayoadhibishwa kila mwaka tarehe 15 Machi;

(c) Kujenga umoja na mshikamano wa kutatua changamoto mtambuka zinazowakabili watumiaji wa Huduma;

(d) Kuwasilisha kwa wadhibiti na Serikalini, maoni mbalimbali yanayokusanywa wakati wa Wiki ya Mtumiaji. Jambo ambalo limerahisisha, usimamizi katika Sekta na kuondoa malalamiko miongoni wa watoa Huduma na watumiaji wa Huduma.

**Ndg. Mgeni Rasmi**

Katika kilele cha maadhimisho, ya mwaka huu, chenye kauli mbiu

"***Akili Mnemba (Artificial Intelligence) inayozingatia Haki na Uwajibikaji wa Mtumiaji"***, kwa pamoja tuliamua kuratibu Mdahalo huu. Hii ni kutokana na umuhimu mkubwa ambao taasisi hizi zinazounda Jukwaa la TCF ziliona ili uelewa wa teknolojia hii ya Akili Mnemba (AI) kuifikia jamii kupitia wadau muhimu katika sekta hizi zinazodhibitiwa na zisizodhibitiwa. Hii itaongeza na kuhakikisha uelewa wa jumla na mapokeo chanya ya matumizi ya teknolojia hii katika kutoa huduma katika nyanja mbalimbali.

**Ndg. Mgeni Rasmi,**

Kama tulivyoeleza awali, kila Mwaka tarehe 15 Machi ni siku ya kilele cha Maadhimisho ya siku ya HAKI ya mtumiaji duniani. Siku hii, chimbuko lake ni la Kihistoria, lililoanzia Nchi za Magharibi (Marekani) Miaka ya 1963. Wakati ule, watumiaji walikuwa wanalipa Huduma na kupata bidhaa kutoka viwandani, ambapo nyingi zilikuwa hazikidhi viwango vya ubora. Sauti zilipazwa, kutetea haki ya mtumiaji dhidi ya wafanyabiashara na watoa Huduma wasiojali maslahi ya watumiaji. Baadae Serikali nyingi Duniani, zilianza kutunga Sheria, na kuunda vyombo vya Kiudhibiti ili kumlinda mtoaji Huduma na mtumiaji Huduma na Bidhaa mbalimbali. Hapa kwetu Tanzania, tuliona Sheria mbalimbali za wadhibiti zipo na ziliundwa na kutoa majukumu mbalimbali kwa Mabaraza ya Watumiaji wa huduma na Bidhaa kama ilivyoelezwa hapo awali.

**Ndg. Mgeni Rasmi**

Pamoja na majukumu mengine ya msingi ya mabaraza haya ni pamoja na kujenga uwezo wa utambuzi wa HAKI za msingi kwa makundi ya rika mbalimbali wakiwemo, watoto, vijana na wazee. Miongoni mwa haki mbalimbali zikiwemo haki ya:

(a) Usalama;
(b) Kupewa taarifa;
(c) Kuchagua;
(d) Kusikilizwa;
(e) Kuelimishwa;
(f) Kupata mahitaji muhimu;
(g) Kulipwa fidia; na
(h) Kutunza mazingira.

**Ndg. Mgeni Rasmi,**

Pamoja na mafanikio na mambo mengi ambayo Jukwaa hili la TCF limeweza kufanikisha, tunakabiliwa na changamoto kadhaa. Moja ya changamoto ya ujumla ni ile ya kukosekana sheria inayowezesha watumia huduma za usafiri majini kuwa na baraza la ushauri la huduma hizo.

Ikizingatiwa jiji la Dar es Salaam ni kitovu cha usafiri wa majini pia ikimaanisha Bandari yetu ya Kimataifa ya Dar es salaam, umuhimu wa kuwa na chombo cha kutetea Haki na Wajibu wa watumia usafiri huu ni muhimu sana katika jitihada za serikali za kuboresha huduma zinazowafikia wananchi.

Hivyo jukwaa la TCF linapenda kukuomba Mkuu wa Mkoa kwa ushawishi wako pia kusaidia kulijengea hoja swala hili ili mchakato wa kulifanikisha ukamilike kwa wakati kupitia taasisi mbalimbali za Serikali.

**Ndg. Mgeni Rasmi**

Kwa pamoja, tunakushukuru sana wewe Binafsi, Makatibu wakuu waliopo hapa, Wenyeviti wote wa taasisi, Wakurugenzi wa Taasisi mbalimbali, wageni wote waalikwa, Mabibi na Mabwana, kwa kukubali kwenu kushiriki nasi katika siku siku hii ya leo.

Mwenyezi Mungu, awabariki na kuwazidishia Neema na Baraka zake.

**Daud G. Daudi**

**MWENYEKITI, JUKWAA LA MTUMIAJI TANZANIA (TCF)**

**15 Machi, 2024**